

Ukiushi wa Kisintaksia katika Tamthiliya ya Kaptula la Marx

Neema George Mturo, PhD.

Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Arusha, Tanzania

Baruapepe: neemamturo@yahoo.com

IKISIRI

Makala haya yanahusu ujitokezaji wa ukiushi wa kisintaksia katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*. Katika makala haya mkabala wa kimaielezo na usampulishaji lengwa ulitumika. Data zilikusanywa kutoka maktabani kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya kusimbisha maudhui. Mjadala wa matokeo ya utafiti umeongozwa na nadharia ya Umitindo iliyoasisiwa na Shykrovsky (1965). Baadae nadharia hii ikaendelezwa na wataalamu wengine kama vile; Leech na Short (2007), Agu (2008) na Wamitila (2008). Makala haya yanaonesha kuna ukiushi wa kisintaksia ambao umekiukwa na mwandishi katika tamthiliya teule. Lengo la kukiuka ni kujenga mtiririko mzuri wa mazungumzo baina ya wahusika katika kujenga visa na matukio ili kuibua maudhui. Aidha Makala haya yanashauri kwa wanafasihi pia kujikita katika tanzu zote za fasihi andishi hasa kwenye tamthiliya ili kuchunguza ukiushi wa darajia ya ushikamani kisarufi na ukiushi wa darajia ya kileksika. Hii ni kutokana na ukweli kwamba ukiushi ndiyo moyo wa ubunifu wenye kudumisha uhai katika tanzu za fasihi.

Maneno ya Msingi: Ukiushi, Sintaksia, Umitindo na Tamthiliya.

DOI: <https://doi.org/10.5281/zenodo.21905706>



This work is licensed under the
Creative Commons Attribution
International License (CC BY 4.0).

Syntactic Deviation in the Play of *Kaptula la Marx*

Neema George Mturo, PhD.

Email: neemamturo@yahoo.com

Tumaini University Makumira, Arusha, Tanzania

ABSTRACT

This article examines the manifestation of syntactic deviation in the play of *Kaptula la Marx*. The study employed a descriptive approach and purposive sampling. Data were collected through library research using textual analysis and analysed through content coding. The discussion of the research findings was guided by the Theory of Stylistics, pioneered by Shykrovsky (1965) and later developed by scholars such as Leech and Short (2007), Agu (2008), and Wamitila (2008). The findings show that the playwright employs syntactic deviation in the selected play. The purpose of this deviation is to create a smooth flow of dialogue among the characters and to develop events and incidents through which various themes are brought to the fore. Therefore, researchers and literary scholars should pay attention to all genres of written literature, particularly drama, in order to examine deviation at the level of grammatical cohesion and lexical deviation. This is because deviation constitutes the heart of creativity and contributes to sustaining the vitality of literary genres.

Keywords: Syntactic deviation, Syntax, Stylistics, Drama.

1. UTANGULIZI

Ukiushi ni dhana ya kimtindo itumikayo katika kazi ya fasihi ambayo ni kinyume na taratibu au kanuni za kawaida zilizozoeleka katika lugha husika. Wapo wataalamu mbalimbali wamefasili dhana ya ukiushi ni kurejelea uteuzi au matumizi ya vipashio vya lugha nje ya taratibu zilizozoeleka (Benpeer, 1986). Naye Mukarovisky (1990) anasema kuwa ukiushi ni upekee unaojitokeza kwenye mtindo. Upekee huo ndio humtofautisha mwandishi mmoja na mwingine. Ukiushi unaweza kuashiria ukuaji wa utanzu wa fasihi kama anavyosema Mohamedi (2001) anaona kuwa utanzu wa fasihi unaopitia ukiushi haubaki vilevile wakati wote bali hubadilika kila siku. Hivyo ukiushi ndio moyo wa ubunifu wenye kudumisha uhai katika tamthiliya. Vilevile tunapochunguza ukiushi katika kazi za fasihi hatuwezi kuepuka vipengele vya mtindo kwenye kazi hizo. Kama anavyoelekeza Enkvist (1999) anaona kuwa mtindo mara nyingi huhusiana na vipengele vya kiisimu ambavyo ni fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki katika muktadha na mazingira ambapo hutokea kwa kuangalia mtindo wa matini.

Njoroge (2017) alishughulikia ukiushi katika tafsiri, Tendwa (2017) alishughulikia ukiushi katika ushairi kwa kuangalia dhana ya mchomozo wa mtindo kwenye diwani ya Andanenga. Pia Wangeci (2018) alichunguza ukiushi katika sanaa ya jumbe cheshi za mtandao. Utanzu wa ushairi ndio ulihusishwa zaidi na ukiushi kutokana na mbinu mbalimbali za kukata maneno, kupindua maneno na kubadili muundo wa tungo katika mshororo ili shairi liweze kuimbika. Kwa upande wa riwaya hutumia lugha ya masimulizi yenye utajiri mkubwa wa sentensi changamano hivyo ukiushi unaweza usiwepo au ukatokea kwa kiasi kidogo. Aidha makala haya yanalenga kuziba pengo ambalo katika utanzu huu wa tamthiliya wengi hawakuweza kumakinikia katika kipengele hiki cha ukiushi wa kisintaksia katika tamthiliya na hasa katika tamthiliya hii ya kaptura la marx. Hivyo makala haya yalikusudia kubainisha ukiushi wa kisintaksia ambao umekiukwa na mwandishi katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*

2. NADHARIA YA UTAFITI

Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Umitindo iliyoasisiwa na Shykrovsky (1965). Baadae nadharia hii ikaendelezwa na wataalamu kama vile:-Leech na Short (2007) wanaeleza kuwa Nadharia ya Umitindo huangazia umuhimu wa lugha katika kuelezea

maana ya matini na pia hutumia kurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani kwa lengo fulani. Wamitila (2008) anasema Nadharia ya Umitindo hutumiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi unaohusisha manufaa ya isimu na huweza kuelezea kama nadharia ambayo iko katikati ya isimu na fasihi. Anasema kuna vipengele vya kimsingi ambavyo vinafaa kuchunguzwa katika kazi ya kifasihi na mhakiki kwa mwelekeo wa uhakiki wa mtindo. Vipengele hivyo ni matumizi ya sentensi fupi na ndefu, uteuzi na mtindo, matumizi ya alama za uandishi, uanafora, kubananga sarufi na mbinu za uwasilishaji wa mawazo. Nadharia ya Umitindo ina mihimili minne ambayo ni muhimili wa Kimofolojia, Kisemantiki, Grafolojia na Kisintakisia. Aidha katika makala haya tumetumia mihimili miwili ambayo ni wa kimofolojia na kisintakisia. Muhimili wa sintaksia umekuwa ni nguzo kwani hushughulikia mpangilio wa maneno katika sentensi kwa kubainisha vijisehemu vyake ambavyo huwa na dhima maalumu. Ukiushi huusisha maswala kama kubananga sarufi na matumizi ya anafora. Kwa ujumla huzingatia ukiushi katika muundo wa kawaida wa matumizi ya sentensi, urefu wa sentensi (fupi au ndefu) na sentensi zenye dosari. Mihimili hii miwili ya nadharia hii imekuwa na ufaafu mkubwa katika makala haya hasa katika muhimili wa sintaksia, muhimili huu umesaidia kubaini ukiushi wa kisintaksia na jinsi ulivyokiukwa na mwandishi katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*. Vilevile ulimsaidia mtafiti kufafanua jinsi ukiushi wa kisintaksia unavyojenga maudhui katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*.

3. METHODOLOJIA ZA UTAFITI

Katika makala haya tumetumia mkabala wa kimaielezo katika kuzichambua data zilizokusanywa kutoka maktabani kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini. Vilevile katika makala haya tumetumia usanifu wa kifani kwa lengo la kubainisha ukiushi wa kisintaksia ulivyokiukwa na mwandishi katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*. Pia utafiti uliofanikisha makala haya ulikuwa ni utafiti wa maktabani. Maktaba zilimuwezesha mtafiti wa makala haya kupata data za upili zinazohusu ukiushi wa kisintaksia ulivyokiukwa na mwandishi katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*. Wango la utafiti katika makala haya ni kazi za mwandishi Kezilahabi.

Katika makala haya mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumika kuteua sampuli. Mtafiti alijiwekea vigezo vitatu ambavyo ni; kwanza matini andishi yenye lugha ya mazungumzo, pili matini rasmi na tatu matini zilizosukwa vizuri na zilizokiuka kanuni

za uandishi wa sarufi ya kiswahili. Utafiti uliofanikisha makala haya ulitumia sampuli ya tamthiliya *Kaptula la Marx* (1999) iliyoandikwa na mwandishi Kezilahabi.

Data za makala haya zilikusanywa kutoka maktabani. Mtafiti alitumia mbinu ya uchanganuzi matini kwa kusoma tamthiliya ya *Kaptula la Marx*. Pia Data zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu za kusimbisha maudhui. Katika makala haya tulizingatia hatua za uchanganuzi wa data. Kwanza kuzizoea data kwa kuzisoma. Data zilikusanywa kutoka kitabu cha tamthiliya ya *Kaptula la Marx*. Pili mtafiti alitengeneza misimbo mbalimbali kwa kuzingatia malengo mahususi, matukio, mipango, maana, uhusiano na hali. Tatu mtafiti aliunganisha misimbo iliyolandana ili kuunda sura fulani ya kimaudhui.

4. MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inawasilisha na kuchambua data zilizokusanywa ili kukidhi lengo la utafiti katika Makala haya. Lengo kuu ni kubainisha ukiushi wa kisintaksia jinsi ulivyokiukwa na mwandishi katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*.

4.1 Kubainisha Ukiushi wa Kisintaksia katika Tamthiliya ya *Kaptula la Marx*

Katika sehemu hii tumejadili na kuwasilisha ukiushi wa kisintaksia ambao umekiukwa na mwandishi katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*. Ukiushi wa kisintaksia uliyobainishwa ni kama ifuatavyo;

4.1.1 Ukiushi wa Miundo ya Tungo

Katika lugha ya Kiswahili tungo hujidhihirisha katika miundo minne ambayo ni; tungo neno, tungo kirai, tungo kishazi na tungo sentensi. Data za utafiti zimebaini kuwa kuna ukiukwaji wa miundo ya tungo katika upangaji wa vipashio vinavyoongana na kujengwa vipashio vikubwa zaidi. Ukiushi wa miundo ya tungo umejitokeza katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx* kama jedwali linavyoonyesha

Jedwali Na.4.1: Ukiushi wa Miundo ya Tungo katika Tamthiliya ya *Kaptura la Marx*

<i>Kaputula la Marx</i>	<i>Ukurasa</i>
Ukiushi wa matumizi ya vielezi katika KT	2,5,10
Ukiushi wa matumizi ya vihusishi katika KT	9,19,30
Ukiushi wa muundo wa Tungo sentensi	5
Ukiushi wa matumizi ya vitenzi vishirikishi katika sentensi	10,12
Ukiushi wa matumizi ya viunganishi katika sentensi	3,9,11,12,17,
Ukiushi wa kitenzi elekezi mara moja	21,27,28 12

Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa kuna ukiukwaji wa miundo ya tungo katika upangaji wa vipashio vinavyoingana na kujenga vipashio vikubwa zaidi. Tungo ni kuweka pamoja au kupanga vipashio sahihi ili kujengwa kipashio kikubwa zaidi. Kama ilivyopendekezwa na Massamba na wenzake (2001) kwamba katika lugha ya kiswahili tungo hujidhihirisha katika miundo minne ambayo ni tungo neno, tungo kirai, tungo kishazi na tungo sentensi. Muhimili huu wa kisintaksia ulituwezesha kubaini miundo mbalimbali ya tungo au sentensi iliyokiukwa na mwandishi wa tamthiliya teule

4.1.1.1 Ukiushi wa Matumizi ya Vielezi katika KT

Katika sintaksia ya Kiswahili kwa kawaida vielezi hujitokeza mara baada ya vitenzi, vivumishi na vielezi vingine. Hufanya kazi ya kufafanua zaidi kielezi au kukumsha kitenzi. Katika utafiti huu data zinaonesha ukiukwaji wa matumizi ya kawaida ya vielezi katika KT. Kwa kutumia mchakato wa kisintaksia wa udondoshaji kwa kudondosha 'T' au mchakato wa upanguaji kwa kubadili nafasi ya 'T' kwenda kwenye nafasi ya 'KE' hivyo, kusababisha KE kujitokeza mwanzoni mwa tungo. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Umitindo, data za *Kaputula la Marx* zinaonyesha kwamba mwandishi ametumia utangulizaji wa virai vielezi kama mkakati wa kuipa taarifa fulani uzito wa kimawasiliano.

4.1.1.1.1 Ukiushi wa Matumizi ya Vielezi katika Tamthiliya ya Kaptula la Marx

Katika tamthiliya ya *Kaputula la Marx* data za utafiti zilizithibitisha dai hili mwandishi anaeleza;

Mfn 1a Mfungwa 2: **Polepole** karatasi nyeupe inaonekana kwenye tundu halafu inaanguka chini (Kezilahabi, 1999: uk 5).

Mfn 1b Mfungwa 6: **Leo jioni** kuna mpira kati ya Mawaziri na Wabunge (Kezilahabi, 1999: uk 27).

Nukuu hapo juu **mfn 1(a)** imeanza na kielezi cha namna (**pole pole, uk 5**) ili kuonesha wazi walipofanikiwa kutoboa tundu ndipo mfungwa namba 6 anaacha kupiga, anakazia macho kwenye tundu. Wenzake wanapomuona nao wanaacha wanatazama tundu, ndio wanaona karatasi nyeupe ikipitishwa polepole kwenye tundu kwa lengo la kuwapasha habari wafungwa ili wajue yanayojili huko nje. Karatasi hiyo wanaipata na mfungwa namba 6 anaanza kuwasomea kwa sauti kubwa kuwa WAFANYAKAZI WOTE DUNIANI UNGANENI. Kadhalika **mfn 1(b)** data inaonesha wazi mwandishi ameanza na kielezi cha wakati (**leo jioni, uk 27**) kwa lengo la kumsisitiza mfungwa namba moja kuangalia mechi kati ya Mawaziri na Wabunge japo yupo gerezeni ili kujua yatakayojili uwanjani kuliko kusubiri kuhadithiwa na mtu mwingine.

Matokea ya data yalionesha kuwa kuna ukiukwaji wa matumizi ya kielezi kwa kujitokeza mwanzoni mwa tungo. Kama ilivyoielezwa na Nduniwe (2020) kuwa kielezi ni neno linalotoa habari juu ya tendo katika sentensi. Kielezi hueleza tendo linafanywa wakati gani, hufanywa wapi, mara ngapi na namna gani. Aidha, kama ilivyofafanuliwa na Wesana- Chomi (2017) anashadadia kuwa vielezi ni neno au fungu la maneno ambalo hufanya kazi ya kufafanua zaidi kielezi au kukumsha kitenzi. Pia Ndung'u (2015) katika makala yake anaeleza kuwa katika sintaksia ya Kiswahili kiambajengo kinachotokea mwanzoni ni nomino au kiwakilishi. Kwa maana hiyo ni vigumu vielezi kujitokeza mwanzoni mwa sentensi. Aidha katika Nadharia ya Umitindo muhimili wa kisintaksia unaeleza kuwa kuna ukiushi wa muundo wa kawaida wa matumizi ya tungo au sentensi. Hivyo makala haya yamebaini ukiushi wa matumizi ya vielezi katika KT kwa kudondosha T na kusababisha kielezi kujitokeza mwanzoni mwa sentensi kwa lengo la

kujenga mtiririko mzuri wa mawazo, visa na matukio katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*.

4.1.1.2 Ukiushi wa Matumizi ya Vihusishi katika KT

Katika sarufi ya Kiswahili vihusishi ni maneno yanayohusisha sehemu mbili au zaidi za sentensi. Kwa kawaida kisintaksia, vihusishi ni kategoria za maneno ambazo huunganisha pamoja vipashio viwili au zaidi visivyo na hadhi sawa. Kimsingi tofauti ya viunganishi na vihusishi ni vipashio vinavyounganishwa. Katika sarufi ya Kiswahili aghalabu kihusishi hakitumiki mwanzoni mwa sentensi. Katika kuthibitisha ukweli wa data za utafiti zilionyesha ukiukwaji wa vihusishi katika KT. Kwa kutumia mchakato wa kisintaksia wa udondoshaji kwa kudondosha 'T' au mchakato wa upanguaji kwa kubadili nafasi ya 'T' kwenda kwenye nafasi ya 'KH' hivyo, kusababisha 'KH' kujitokeza mwanzoni mwa sentensi. Matumizi haya ya ukiukwaji wa vihusishi katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx* yamejitokeza kama ifuatavyo: -

4.1.1.2.1 Ukiushi wa Matumizi ya Vihusishi katika Tamthiliya ya *Kaptula la Marx*.

Data zimeonyesha kuna ukiukwaji wa matumizi ya vihusishi katika KT kwenye tamthiliya ya *Kaptula la Marx*, aidha ukiukwaji huo hujitokeza mwanzoni mwa sentensi. Mwandishi anathibitisha hili kwa kusema;

Mfn 2a Rais Kapera: ***Karibu na jela*** ya wafungwa wa kisiasa
(Kwa sauti ya juu) Wapime mwamko. (Kezilahabi, 1999: uk 30).

Mfn 2b Waziri wa Mambo ya Ndani: ***Kwa muda*** wa miezi mitatu
iliyopita, kulikuwa na hatari ya kupinduliwa.
(Kezilahabi, 1999: uk 9).

Mfn 2(a) ulionyesha ukiukwaji wa matumizi ya kihusishi cha mahali (**karibu na jela, uk 30**) kwa ajili ya kuonesha sehemu ambayo Rais Kapera alikokuwa anaua watu wanaoenda kinyume na uongozi wake. Rais Kapera anamwambia daktari akishindwa kuwapima wananchi wake mwamko wa kisiasa kesho kunguru watarukaruka juu ya kichwa chake katika bonde la Udongo- Kwimana. **Mfn 2(b)** hapo juu kihusishi cha

wakati (**kwa muda, uk 9**) kimejitokeza mwanzoni mwa sentensi kuonesha jinsi katika uongozi wa Rais Kapera kulikuwa na hatari ya kupinduliwa lakini vijana wetu wanaotambaa waligundua mpango huu mapema hivyo kwa sasa nchi iko salama kabisa hasiwe na hofu. Kwa kuzingatia nukuu hiyo matokeo yalionesha kuna ukiukwaji wa matumizi ya vihusishi katika tungo au sentensi.

Ipara (2010) anashadadia kuwa kigezo cha sintaksia kinatuonesha kuwa vihusishi mara nyingi hufuatiwa na nomino au kiwakiishi kama vile; la kaka, za kwetu, la kwake na la moto. Pia huweza kutanguliwa na nomino, viwakilishi, vivumishi, vitenzi na vielezi na hufuatiwa na nomino au kiwakiishi. Hii ina maana kwamba, sio rahisi katika muundo wa kiswahili kuanza na kihusishi au kuishia na kihusishi. Muhimili wa kisintaksia ambao unashughulikia mpangilio wa maneno katika sentensi kwa kubainisha vijisehemu vyake ambavyo huwa na dhima maalumu katika nadharia ya umitindo umetusaidia kubaini ukiushi wa matumizi ya vihusishi. Kwa mintarafu hii makala haya yamebaini ukiushi wa matumizi ya vihusishi kwa kujitokeza mwanzoni mwa sentensi. Watunzi wanapofanya hivi huwa na lengo la kuipa sentensi uzito usio wa kawaida kwa lengo la kusesitiza jambo analokusudia kwa hadhira yake.

4.1.1.3 Ukiushi wa Muundo wa Tungo Sentensi

Katika sintaksia ya Kiswahili muundo wa kawaida wa sentensi ni KN+KT. Mwandishi katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx* anakiuka kanuni hii kwa kutumia mchakato wa kisintaksia wa udondoshaji kwa kudondosha ‘KN’. Hivyo kusababisha ‘KT’ kujitokeza mwanzoni mwa tungo sentensi. Katika sehemu inayofuata tunaonesha ukiushi wa tungo sentensi katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*

4.1.1.3.1 Ukiushi wa Miundo ya Tungo Sentensi katika Tamthiliya ya Kaptula la Marx

Data zimebaini kuna ukiukwaji wa muundo wa tungo sentensi kwa kuanza na ‘KT’ kwa kudondosha ‘KN’ katika tamthiliya hii ya *Kaptula la Marx*:-Mwandishi anathibitisha hili;

Mfn 3a Mfungwa 6: **Tukitoka** jela tutasimamia haki na
maendeleo ya wakulima na wafanyakazi
Wote: (Wanarudia)

Mfungwa 6: **Tukitoka** jela tutahakikisha kwamba, hakuna namna yoyote ya dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu au upendeleo!

Wote: (Wanarudia)

Mfungwa 6: **Tukitoka** jela tutakomesha uongozi wa kinafiki!

Wote: (Wanarudia). (Kezilahabi, 1999: Uk 5).

Nukuu hapo juu data za utafiti katika makala haya zinaonesha ukiushi wa muundo wa tungo sentensi kwa kudondosha 'KN' ili kuonesha hasira walionayo wafungwa kutokana na ukosefu wa haki na usawa katika nchi moja barani Afrika. Wananchi wanaonewa, wananyanyaswa na kukandamizwa hivyo wafungwa gerezeni wanapambana ili wafanikiwe kutoka nje kwa lengo la kukomesha ukosefu wa haki na usawa miongoni mwa wananchi.

Matokeo ya data yanaonesha kuwa kuna ukiushi wa muundo wa tungo sentensi kwa kuanza na **KT** badala ya **KN**. Kama ilivyofafanuliwa na Khamis na Kiango (2002) kuwa tungo sentensi ni kipashio cha juu kabisa katika tungo chenye muundo wa kiima na kiarifu ambacho hutoa taarifa kamili. Katika lugha ya kiswahili muundo wa sentensi kwa kawaida huundwa na KN na KT. Nadharia ya Umitindo muhimili wa kisintaksia unadai kuwa kuna ukiushi wa muundo wa kawaida wa matumizi ya tungo au sentensi. Ukiushi wa muundo wa tungo sentensi ni miongoni mwa mbinu muhimu katika nadharia ya umitindo na ukiushi huu umebainika katika tamthiliya teule. Matokeo ya data za utafiti yamebainisha ukiushi wa muundo wa sentensi iliyozeleka kwa kudondosha KN. Katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*. Mwandishi amefanya hivi kwa makusudi maalumu kwa lengo la kufikisha ujumbe aliokusudia kwa jamii inayomzunguka.

4.1.1.4 Ukiushi wa Vitenzi Vishirikishi (t) katika Sentensi

Kwenye lugha ya Kiswahili Vitenzi vishirikishi (t) vinaashiria kihali, kitabia au kimazingira. Katika muundo ya lugha ya Kiswahili sentensi huundwa na KN+KT lakini mwandishi anakiuka matumizi sahihi ya vitenzi vishirikishi kwa kutumia mchakato wa kisintaksia wa udondoshaji kwa kudondosha 'KN'. Hivyo, kusababisha kitenzi kishirikishi (t) kujitokeza mwanzoni mwa sentensi. Mwandishi anakiuka taratibu za vitenzi vishirikishi zilizozoeleka kwa kuanza na kitenzi kishirikishi mwanzoni mwa sentensi kama ifuatavyo

4.1.1.4.1 Ukiushi wa Matumizi ya Vitenzi Vishirikishi katika Tamthiliya ya Kaptula la Marx

Data za utafiti katika makala haya zimebaini kuna ukiukwaji wa vitenzi vishirikishi katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx*, mwandishi anathibitisha dai hili anasema;

Mfn 4a Rais Kapera: *Ni mtu hatari sana! anafikiri sana na amesoma sana Marx na Lenini. Mchungeni.* (Kezilahabi, 1999: uk 10).

Mfn 4b Rais Kapera: *Ni Pana sana na refu. Linakaribia kufunika Kaputula* (Kezilahabi, 1999: uk 12).

Mfn 4c Rais Kapera: *Hili gwanda lilikuwa likivaliwa na rafiki yangu. Ni marehemu sasa.* (Kezilahabi, 1999: uk 12).

Katika **Mfn 4 (a)** hapo juu kitenzi kishirikishi cha uyakinishi (**ni uk 10**) kimetumika mwanzoni mwa sentensi. Data hii ilitibitisha kitenzi kishirikishi kujitokeza mwanzoni mwa sentensi ili kuonesha hali ya hofu aliyokuwa nayo Rais Kapera kwa Mzee Mwangaza Africanus kuwa ni mtu hatari sana na amesoma sana Marx na Lenini hivyo anamuagiza Waziri wa Mambo ya Ndani amchunge sana.

Hali kadharika **mfn 4(b)** hapo juu unaonesha kitenzi kishirikishi cha uyakinishi (**ni uk 12**) kujitokeza mwanzoni mwa sentensi kuonesha msisitizo kuwa Rais Kapera anang'ang'ania kuvaa mavazi ambayo hayamtoshi aliyoyaiga kutoka nchi za baridi. **mfn 4 (c)** hapo juu unaonesha kitenzi kishirikishi cha uyakinishi (**ni uk 12**) kuanza mwanzoni mwa sentensi ili kuonesha magwanda anayovaa Rais Kapera yalikuwa yanapendwa kuvaliwa na rafiki yake ambaye kwa sasa ni marehemu. Makala haya yalionesha kuwa kuna ukiushi wa vitenzi vishirikishi kwa kujitokeza mwanzoni mwa sentensi. Vitenzi vishirikishi hufanya kazi ya kuunganisha sehemu mbili katika sentensi. Pia katika kazi ya Njogu na Chimerah (2006) walizungumzia kuwa katika lugha ya Kiswahili vitenzi vishirikishi vinaashiria kihali, kitabia na kimazingira kwa maana hiyo katika sintaksia ya Kiswahili si rahisi vitenzi vishirikishi kujitokeza mwanzoni mwa sentensi. Katika makala haya tumebaini kuwa kuna ukiushi wa matumizi ya vitenzi vishirikishi katika sentensi kwa kudondosha KN hivyo kusababisha KT kujitokeza mwanzoni mwa sentensi. Mwaandishi wa tamthiliya teule amefanya hivi ili kuonesha hali, mazingira, na tabia mbalimbali zilizoibuka katika jamii inayomzunguka.

4.1.1.5 Ukiushi wa Matumizi ya Viunganishi katika Sentensi

Katika sintaksia ya Kiswahili viunganishi hutumika kuunganisha neno na neno, kirai na kirai, kishazi na kishazi au sentensi na sentensi. Kwa kawaida, kisintaksia viunganishi huunganisha vipashio viwili au zaidi vyenye hadhi sawa. Katika makala haya data zinaonesha ukiukwaji wa matumizi ya viunganishi kwa kudondosha kipashio kimoja au zaidi katika sentensi hivyo kusababisha kiunganishi kuja kukaa mwanzoni mwa sentensi. Katika sehemu inayofuata tunabainisha aina za viunganishi vilivyokiukwa

4.1.1.5.1 Ukiushi wa Matumizi ya Viunganishi katika Tamthiliya ya *Kaputula la Marx*.

Data za utafiti katika makala haya zime *kuhadaa*. (Kezilahabi, 1999: uk 28).bainisha kuna ukiukwaji wa viunganishi katika *tamthiliya ya Kaputula la Marx* mwandishi anathibitisha hili anasema;

Mfn 5a Mfungwa 1: ***Kama*** mbuzi vile! wengi sana! Kila mahali
(Kezilahabi, 1999: uk 3).

Mfn 5b Mfungwa 6: ***Na*** Yale madebe ni yetu (Kezilahabi, 1999: uk 17).

Mfn 5c Mkulima: ***Na*** Mimi unikumbuke kwenye ufalme wako wa
usawa (Kezilahabi, 1999: uk 21).

Mfn 5d Sauti 1: ***Na*** huyo Waziri wa zamani amepewa adhabu gani
(Kezilahabi, 1999: uk 27).

Mfn 5e Sauti 1: ***Na*** kipofu anayeona ni hatari zaidi! Anaweza sana
kuhadaa. (Kezilahabi, 1999: uk 28).

Mfn 5f Waziri wa Mambo ya Ndani: ***Lakini*** vijana wanaotambaa
waligundua mpango huo mapema.
(Kezilahabi, 1999: uk 9).

Mfn 5g Tarishi: ***Lakini*** Mzee hayakutoshi hayo mavazi. (Kezilahabi,
1999: uk 12).

Mfn 5a hapo juu kiunganishi kiongezi (**kama uk 3**) kimejitokeza mwanzoni mwa sentensi kuonesha kuwa mfungwa namba moja amefungiwa ndani muda mrefu. Macho yake yanapoteza uwezo wa kuona vizuri hivyo hana uhakika wa kile anachokiona. Tena **mfn 5b** hapo juu umeanza na kiunganishi kiongezi (**na uk 17**) kuonesha msisitizo kuwa sisi ni wafungwa hivyo tunahitaji kufanya jitihada za kujikomboa kutoka kifungoni. Vilevile **mfn 5c** hapo juu kiunganishi kiongezi (**na uk 21**) kimejitokeza

mwanzoni ili kumsisitiza Rais Kapera amkumbuke mkulima kwenye ufalme wa usawa akiwa na maana ya kumkomboa mkulima kutoka kwenye hali duni ya umaskini.

Tena **mfn 5d** hapo juu nukuu imeanza na kiunganishi kiongezi (**na uk 27**) kwa lengo la kuuliza swali ili kuonesha uongozi wa Rais Kapera ulivyokuwa unaua watu kikatili wanaoenda kinyume na matakwa yake. Halikadharika **mfn 5e** hapo juu unakiuka taratibu za matumizi ya kawaida ya kiunganishi kiongezi (**na uk 28**) ili kuonesha jinsi tabaka tawala linavyokandamiza tabaka la chini. Ingawa tabaka la chini linaona vitendo vya unyanyasaji na ukatili wanaofanyiwa na tabaka la juu ila wanakaa kimya kama vipofu, lakini mwandishi anasisitiza kipofu anayeona ni hatari sana maana siku akichoka basi nchi itageuka bahari ya damu.

Ingawa **mfn 5f** hapo juu unaanza na kiunganishi kichaguzi (**lakini uk 9**) kuonesha usalama wa nchi ya Rais Kapera kuwa hakuna shida yoyote. Nchi ni salama kwenye kila eneo hivyo Rais Kapera asiwe na wasiwasi kuhusu nchi yake wala uongozi wake. Kutokana **Mfn 5g** hapo juu kiunganishi kichaguzi (**lakini uk 12**) kimejitokeza mwanzoni kumuonesha Tarishi kutoridhishwa na mavazi ya Rais Kapera. Hivyo anamsisitiza Rais Kapera kuachana na mavazi aliyoyaiga kutoka nchi za baridi.

Aidha matokeo ya data yalionesha kwamba kuna ukiushi wa matumizi ya viunganishi kwa kujitokeza mwanzoni mwa sentensi. Viunganishi ni maneno ambayo huunganisha maneno au fungu la maneno. Shabani (2013) anatanabahisha kuwa dhima ya viunganishi hutumika kuunganisha vipashio viwili au zaidi vyenye hadhi sawa. Hivyo sio rahisi viunganishi kujitokeza mwanzoni au mwishoni katika sentensi. Matokeo ya utafiti huu yamebaini ukiushi wa matumizi ya viunganishi katika sentensi kwa kudodosha kipashio kimoja au viwili katika sentensi. Mfano, katika *Kaptula la Marx*; *Na kipofu anayeona ni hatari zaidi! Anaweza sana kuhadaa.* Katika Mfano huo umeonesha udondoshaji wa kipashio kimoja au viwili.

4.1.1.6 Ukiushi wa Vitenzi Elekezi Mara Moja katika Sentensi

Sintaksia ya Kiswahili vitenzi elekezi mara moja huwa ni vitenzi vyenye kubeba yambwa moja tu. Mwandishi wa tamthiliya ya *Kaptula la Marx* anakiuka kanuni hii kwa kudondosha '**yambwa**'.

4.1.1.6.1 Ukiushi wa Kitenzi Elekezi Mara Moja katika Tamthiliya ya Kaptula la Marx

Katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx* mwandishi amekiuka muundo wa kitenzi elekezi mara moja katika sentensi. Data za utafiti zilionesha kuna ukiukwaji wa muundo wa kitenzi elekezi mara moja kwa kudondosha yambwa. Mfano wa data hapo chini inaonesha dai hili;

Rais Kapera: *Rais Kapera analivaa*. (Kezilahabi, 1999: uk 12).

Nukuu hapo juu katika data za utafiti zinaonesha ukiushi wa wa muundo wa kitenzi elekezi mara moja kwa kudondosha **yambwa**. Aidha Mwandishi amefanya hivi ili kutumia lugha fiche kutokana na kuwepo kwa vuguvugu la siasa ya ujamaa. Hivyo, mwandishi anaficha dhihaka yake kwa Rais Kapera kwa kung'ang'ania kuvaa kaptula ambalo halimtoshi.

Kwa kuzingatia nukuu hiyo hapo juu matokeo yalionesha kuna ukiukwaji wa vitenzi elekezi mara moja. Kama ilivyofafanuliwa na Rubanza (2003) kuwa vitenzi elekezi ni vitenzi vinavyohitaji kujalizwa na nomino moja au mbili. Habwe na Karanja (2004) wanashadadia kuna aina mbili za vielezi kwa kigezo cha uelekezi. Matokeo ya data yamebaini kuwa usimulizi wa tamthiliya ni wa majibizano baina ya wahusika mbalimbali, ndio maana ukiushi wa kisintaksia unaonekana kwa wingi kwa lengo la kujenga mtiririko wa mazungumzo kati ya muhusika mmoja na mwingine ili kujenga visa na matukio hivyo kumfanya msomaji kuibua taharuki, kuvuta hisia na kuibua udadisi kwa msomaji.

5. Hitimisho

Kwa ujumla katika makala haya matokeo yameonyesha kuwa ukiushi wa kisintaksia ulivyokiuka na mwandishi ulikuwa na lengo la kusawiri mambo yaliyopo kwenye jamii kama vile; uongozi mbaya, unyanyasaji, ukandamizaji, kejeli, ukosefu wa haki na matabaka. Vilevile mwandishi alikiuka kaida au taratibu za lugha zilizozoeleka ili kufikisha ujumbe uliokusudia kwa jamii inayomzunguka kwa lengo la kuonya, kuelimisha na kuburudisha jamii. Makala haya yanapendekeza kuwa watafiti na wataalamu wa fasihi wanapaswa kujikita katika tanzu zote za fasihi andishi hasa kwenye

tamthiliya ili kuchunguza ukiushi wa darajia ya ushikamani kisarufi na ukiushi wa darajia ya kileskika. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, ukiushi ndio moyo wa ubunifu wenye kudumisha uhai katika tanzu za fasihi.

MAREJELEO

- Agu, I. (2008). *A linguistic Stylistic Analysis of Sonyinka*. Yola: Federal University of Technology Press.
- Benpeer, C. (1986). *Essays in Modern Stylistics*. London: Oxford University Press.
- Enkvist, N. (1999). *Linguistics and style*. London: Oxford University Press.
- Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Msingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publisher Ltd.
- Ipara, I. (2010). *Upeo wa Sarufi Kwa Shule za Upili*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kezilahabi, E. (1999). *Tamthiliya ya Kaputula la Marx*. Dar es Salaam: DUP Limited.
- Khamis, A. M. & Kiango, J.G. (2002). *Uchanganuzi wa Sarufi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KIUTA.
- Kihore, Y. M. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Sanifu 2*. Dar es Salaam: TUKI.
- Leech, G. & Short M. (2007). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*. Toleo la Pili. Harlow: Longman Group Limited.
- Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M. & Hokororo, J.I. (2001). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu Sekondari na Vyuo*. Dar es salaam: TUKI.
- Matei, A. K. (2008). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Education Publishers.
- Mohamed, M. A. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mturo, N. G. (2017). *Kitanzi*. Dar es Salaam: B&L International Ltd.
- Mukarovisky, J. (1990). *Standard Language and Poetry Language*. Washton DC: Georgetown University press.
- Ndumiwe, E. J. (2020). *Kurunzi ya Isimu na Muundo wa Kiswahili*. Mwanza: Tridax Africa Company Limited.
- Ndung'u, N. M. (2015). 'Information Structure in Kiswahili'. *International Journal of Education and Research*, 3 (3): 309- 320.
- Njogu, K., Mwihi, A. & Buliba, A. (2006). *Sarufi ya Kiswahili: Uchanganuzi na Matumizi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njoroge, K. (2017). "Ukiushi katika Tafsiri". *Tasnifu ya Uzamili (Haijachapichwa) Chuo Kikuu Cha Nairobi*. Kenya.

- Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.
- Rubanza, Y. I. (2003) *Sarufi: Mtazamo wa kimuundo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Shabani, N. (2013). *Nadharia ya Sarufi*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Shyklovsky, V. (1965). *Arts as technique*. NE: University of Nebraska Press.
- Tendwa, A. (2017). "Mchomozo katika Fasihi ya Kiswahili". Tasnifu ya Uzamili (Haijachapwa) Chuo Kikuu Huria. Tanzania.
- Wamitila, K. (2008). *Kazi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers Limited.
- Wangepi, W. (2017). "Ukiushi wa Kiisimu katika Jumbe cheshi za Mtandao". Tasnifu ya Uzamili (Haijachapwa) Chuo Kikuu Cha Moi. Kenya.
- Wesana- Chomi, E. (2017). *Kitangulizi cha Muundo, Viambajengo na Sentensi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TATAKI.